TANZANIA HEART INSTITUTE

"From the Heart for the Heart"

www.tanzaniaheartinstitute.org

TAARIFA FUPI YA MAENDELEO YA TAASISI YA TIBA YA MAGONJWA YA MOYO *TANZANIA (TANZANIA HEART INSTITUTE- THI)* KWA KAMATI BUNGE YA HUDUMA ZA JAMII

Kwanza napenda kutoa shukrani zangu kwa Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii ya Bunge la Jamhuri ya Muungano Tanzania, kwa kunipatia nafasi ya kuongea na kuelezea kuhusu Taasisi ya Tiba ya Magonjwa ya Moyo Tanzania (THI) wakati wa Kikao cha Bunge la Bajeti mjini Dodoma Jumatano, tarehe 25 Juni, 2008.

1.0 HISTORIA YA TAASISI YA TIBA YA MAGONJWA YA MOYO TANZANIA *(TANZANIA HEART INSTITUTE - THI)*

1.1 Taasisi ya Tiba ya Magonjwa ya Moyo ilianzishwa na Dr. Ferdinand B. Masau wakati akiwa masomoni nchini Marekani katika Taasisi ya Tiba ya Magonjwa ya Moyo ya Texas *(Texas Heart Institute)* chini ya udhamini wa Chuo Kikuu cha Texas *(University of Texas Health Science Center-Houston)* na Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia ya Tanzania. Taasisi iliandikishwa rasmi nchini Marekani June, 1999 na kupewa msamaha wa kodi nchini Marekani *(Non Profit Tax Exempted Organization).*

1.2 Ni vizuri kufahamu kuwa juhudi za Dr. Masau kuanzisha huduma ya upasuaji wa moyo hapa nchini zilianza mwaka 1992 akiwa masomoni nchini China wakati akisomea Shahada ya Udhamili katika Upasuaji wa Kifua, Moyo na Mishipa ya Damu. Juhudi hizo hazikuzaa matunda katika kuishawishi Hospitali ya Muhimbili (alikokuwa anafanyia kazi wakati huo). Pia alijaribu kuushawishi uongozi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili na hospitali zingine kama KCMC, Bugando, Mikocheni Mission Hospital, na Tumaini Hospital ya mjini Dar-es-Salaam akiwa masomoni nchini Marekani kati ya 1997 na 2000 (kwa kufunga safari na kuja hapa nchini kwenye hizi hospitali kwa majadiliano) lakini ilishindikana. Ni hospitali ya TMJ Hospital iliyoko Dar-es-Salaam iliyokubali na kutoa ushirikiano na kumwezesha Dr. Masau kuja kuanzisha Huduma ya Upasuaji wa Moyo hapa nchini.

1.3 Dr. Ferdinand Masau ni mwanachama wa Chama cha Tiba ya Upasuaji wa Kifua na Moyo Duniani *(The Society of Thoracic Surgeons)* na amekuwa

mmoja wa viongozi wa Chama hicho tangu mwaka 2000 hadi 2008 akiwa mjumbe katika Kamati maalum inayoshughulikia mahusiano ya Kimataifa *(Workforce on International Relationships of the Society of Thoracic Surgeons).*

Pia Dr. Ferdinand Masau ni Mwanachama Mwanzilishi na mmoja Viongozi wa Program inayoratibu Huduma ya Upasuaji wa Moyo Duniani *(Founding Member of the International Cardiac Surgery Outreach Program)* chini ya Shirikisho la Moyo Duniani *(World Heart Foundation).*

1.4 Taasisi ya Tiba ya Magonjwa ya Moyo Tanzania ilianza rasmi kazi nchini Tanzania baada ya kutambuliwa na kupewa kibali kama hospitali na Wizara ya Afya tarehe 15 Mei, 2002. Pamoja na kushughulikia tiba ya magonjwa ya moyo, Taasisi pia inashughulikia kutoa tiba ya magonjwa mengine. Lengo hasa ni kuwa na taasisi iliyo na uwezo wa kutoa huduma katika nyanja tatu kubwa:

- **Tiba ya magonjwa ya moyo,**
- **Utafiti katika nyanja zinazohusiana na magonjwa ya moyo, na**
- **Kutoa elimu na ufundishaji wa Wataalam mbalimbali kuhusiana na tiba ya magonjwa ya moyo**.

2.0 KUIMARISHA HUDUMA ZA TAASISI

Kwa sasa hivi Taasisi iko katika kumalizia hatua ya kwanza *(PHASE I)* ya kuweka msingi wa kuweza kutoa huduma inayofaa na bora ya tiba ya magonjwa ya moyo. Hatua inayofuatia ni kuboresha na kupanua shughuli za Taasisi hasa katika tiba na utafiti.

2.1 Pamoja na kutoa huduma ya tiba kwa wagonjwa mbalimbali wa moyo, Taasisi imefanikiwa kufanya jumla ya operesheni zaidi ya 100 za upasuaji mkubwa wa moyo kama vile kuweka *valve* mpya *(Valve Replacement).* Taasisi inatazamia kufanya operesheni nyingi zaidi iwapo itapata wagonjwa wanaofadhiliwa na Serikali badala ya kuwapeleka nje ya nchi kama ilivyo sasa.

Taasisi ya Tiba ina wajumbe kumi na wawili (12) wa Bodi ya Wakurugenzi ambapo sita ni Watanzania, wanne kutoka Marekani na wawili kutoka Ujerumani.

2.2 Juhudi za kuijenga na kuimarisha Taasisi zinafanywa. Hii ni pamoja na jitihada za kutafuta wataalam waliobobea katika kutoa tiba ya magonjwa ya moyo. Katika kufanikisha hili Taasisi yetu imefanikiwa kufikia

makubaliano na Shirika la Kijerumani la **SES,** ambapo Shirika hilo linagharamia na kuleta Wataalam waliobobea wa Kijerumani kuja kutoa ushauri, kufundisha na kuimarisha utoaji wa huduma mbalimbali katika Taasisi yetu. Wataalam hao hukaa kwa mzunguko wa miezi sita. Tayari Shirika hilo lilishaleta Wataalam wanne na ambapo wawili kati yao walisaidia kutoa ushari wa ujenzi wa hospitali mpya ya THI iliyoko katika majengo ya NSSF pale ilipokuwa TAZARA Hosteli na kufundisha Wafanyakazi wa THI katika nyanja zao.

2.3 **Juhudi zaidi zimefanywa kupata misaada ya kuiimarisha Taasisi kutoka ndani na nje ya nchi.** Mazungumzo na makubaliano yalifikiwa na Mkataba kutayarishwa (MOU) kati ya Taasisi ya Tiba ya Magonjwa ya Moyo ya Ujerumani-Munich na Voelklingen *(German Heart Centre-Munich and German Heart Centre-Voelklingen),* Wizara ya Afya na Taasisi yetu, ambapo Taasisi hizo za Ujerumani zitakuwa zinaleta timu ya Wataalaam wa upasuaji wa moyo kuja kusaidia kutoa huduma ya upasuaji wa moyo hapa kwenye Taasisi yetu; kutoa vifaa mbalimbali na kutoa mafunzo kwa Wafanyakazi wazalendo na wengine kuwapeleka kwenda kwenye mafunzo zaidi nchini Ujerumani. Tayari kwa kupitia Taasisi hizo za Ujerumani, Mashirika maalum yameundwa (*Heart to Heart Foundation* na *Heart for Tanzania)* kwa ajili ya kugharamia mafunzo kwa Wafanyakazi wa Taasisi kwenda kusoma Ujerumani, kugharamia Wataalam kutoka Ujerumani na pia baadhi ya fedha kusadia kugharamia upasuaji wa moyo kwa wagonjwa wasiojiweza. Tayari Euro 300,000 zimechangwa na familia moja ya Ujerumani kwa ajili hiyo. Hatua inayofatia ni kusaini Mkataba ili yote hayo yatekelezwe (angalia viambatanishi).

2.4 Katika kufanikisha hili Taasisi ya Moyo ya Ujerumani mjini Munich ilimwalika Dr. Ferdinand B. Masau, Mwanzilishi na Mkuu wa Taasisi ya THI kuhudhuria mazungumzo na majadiliano kati ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii wa Tanzania na Wakuu wa Taasisi hiyo ya Kijerumani mjini Munich. Mazungumzo hayo yalifanyika tarehe 15 Oktoba, 2003. Lengo la Taasisi hiyo ni kutoa misaada mbalimbali kwa THI ya kiufundi, Wataalam na fedha iwapo Serikali kwa kupitia Wizara ya Afya itatoa baraka na kukubali misaada hiyo itolewe kwa taasisi yetu ya THI. Hii ni pamoja na kukubali wagonjwa wanaotakiwa kupata huduma ya upasuaji wa moyo watibiwe katika hospitali yetu badala ya kuwapeleka nje ya nchi.

Taasisi hizo za Ujerumani ziko tayari kutoa timu ya Wataalaam kuja na kutoa huduma hiyo kwa wagonjwa wanaofadhiliwa na Serikali.

2.5 Pia Wataalam kutoka nchini Uingereza katika Taasisi ya Tiba ya Magonjwa ya Moyo ya Oxford na Hospitali ya Radicliffe mjini *London (Oxford Heart Centre and John Radicliffe Hospital, London)* licha ya kuingia mkataba na

Dr. Masau/THI pia walishamwandikia Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, wakiomba ushirikiano wake kwa niaba ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Uingereza ili Wataalam hao waweze kuisaidia Taasisi ya Moyo Tanzania ili iweze kufikia malengo yake ya kutoa tiba ya magonjwa ya moyo nchini.

2.6 Taasisi yetu hivi sasa inafanyakazi kwa kushirikiana na Shirikisho la Utoaji wa Tiba ya Magonjwa ya Moyo Duniani **(THI is officially affiliated to the World Heart Foundation).** Napenda kuchukua nafasi hii kukutaarifu kuwa Rais wa Shirikisho hilo, Dr. Thomas Pezella aliwasili hapa nchini mwezi Machi, 2004. Wakati wa ziara yake hiyo aliandamana na Wataalam wengine wa moyo na walishiriki kufanya operesheni mbalimbali za moyo katika Taasisi ya Magonjwa ya Moyo ya Tanzania (THI). Pia wataalam hawa walipata nafasi ya kukutana na viongozi wa Wizara ya Afya na wadau wengine.

3.0 VIFAA NA MISAADA

3.1 Taasisi yetu inatazamia kuongeza na kuboresha huduma zake kwa kuongeza vifaa vya kisasa na muhimu kama *Catheterization Unit* (Mitambo na vifaa vya kupimia mishipa ya Damu kwenye Moyo, Ubongo, n.k.), *TEE* (*Transesophageal Echo* – Upimaji wa Moyo kupitia koo la chakula), n.k. Kwa sasa hivi Taasisi yetu ina vifaa vyenye thamani ya sh. bilioni kumi. Hii inaifanya Taasisi yetu kuwa moja ya Taasisi zenye vifaa vyenye gharama kubwa hapa nchini. Thamani ya vifaa vyetu itaongezeka na kufikia sh. bilioni kumi na mbili ifikapo mwishoni mwa mwaka huu. Wataalaam kutoka *Biomedical Engineering Department* ya *Texas Heart Institute* na *Texas Children's Hospital* huja mara mbili kwa mwaka kuja kuangalia na ku-*service* vifaa vyetu.

3.2 Tunapenda kutoa shukrani kwa Taasisi mbalimbali za ndani, ambazo zimejenga ushirikiano na Taasisi yetu kama NSSF, n.k. kwani Taasisi hizi zinajitahidi kuijenga na kuisimamisha Taasisi yetu katika misingi imara. Aidha, tunatoa shukrani kwa watu binafsi ambao wamekuwa wanatusaidia kwa misaada mbalimbali kwa njia moja au nyingine.

3.3 Taasisi ya Tiba ya Magonjwa ya Moyo Tanzania (THI) itakuwa mwenyeji wa Semina ya Tano ya Tiba ya Magonjwa ya Moyo katika Bara la Afrika *(The 5th African Heart Seminar)* itakayofanyika kuanzia tarehe 18 hadi 23 Julai, 2008. Hii ni mara ya kwanza kwa semina ya aina hii kufanyika hapa nchini. Wakati wa semina hii mafunzo ya nadharia na vitendo yatatolewa kwa washiriki. Pia wakati wa semina hii operesheni za moyo zitafanyika na kuonyeshwa kupitia vituo vya Elimu ya Mtandao vya Benki ya Dunia katika nchi mbalimbali duniani.

4.0 CHANGAMOTO

4.1 Pamoja na jitihada zote hizo za kuijenga na kuisimamisha Taasisi yetu, bado THI inakabiliana na changamoto mbalimbali hasa katika kupata fedha za kuendeshea Taasisi kutoka ndani ya nchi. Tunaomba msaada wa fedha kutoka kwa Mashirika, Makampuni na watu binafsi ili tusaidiwe kuisimamisha na kuijenga Taasisi hii.

Na kubwa zaidi ili kuijenga na kuisimamisha taasisi hii tunaomba:

4.2 Wizara ya Afya kuridhia na kusahini Mikataba iliyoainishwa hapo juu ili Taasisi hizo ziweze kuleta Wataalam, vifaa na fedha kwa ajili ya kuimarisha huduma ya tiba ya magonjwa ya moyo. THI inaiomba na kuishawishi Serikali ilete wagonjwa watibiwe katika hospitali hii, badala ya kuwapeleka katika hospitali za nje. Kwa kufanya hivyo, Wataalam hawa kutoka nje watasadia kuwaelimisha Wataalam wetu wa Kitanzania na kupunguza gharama ya kuwapeleka nje kujifunza. Aidha, kwa kutowapeleka wagonjwa nje ya nchi, Serikali itaokoa fedha nyingi na wakati huo huo Wataalam wazalendo watapata ujuzi na uzoefu wa kazi zao na pia itasaidia Wataalam wazalendo wasikimbilie nchi za nje *(BRAIN DRAIN).*

4.3 Gharama ya pango (mali ya NSSF) ni kubwa kwa Taasisi na ni mzigo mkubwa. Taasisi haijawa na uwezo wa kulipa gharama hii ya pango ambayo ni kubwa sana (Tsh. Milioni 800 kwa mwaka). Mzigo huu unaweza kupunguzwa kwa kiasi kikubwa kwa Wizara ya Afya kuridhia kusaini Mikataba iliyoainishwa hapo juu, na Serikali kuleta wagonjwa kutibiwa katika Taasisi hii. Aidha, NSSF kukamilisha ukarabati wa ujenzi wa majengo ya hospitali kama ilivyo katika Mkataba. Taasisi zinazoshirikiana na THI kwa ufadhili zinataka ukarabati huo ukamilike kama ilivyo katika michoro ya majengo iliyoidhinishwa wakati wa majadiliano na makubaliano. Kwa mfano ICU imewekwa ghorofa ya kwanza badala ya *ground floor*, *lift* ni ndogo kiasi kwamba hairuhusu kupitisha mgonjwa aliye kwenye kitanda wanaomuhudumia, na hakuna choo OPD kama ilivyo kwenye michoro, n.k.

5.0 MAOMBI YA TAASISI KWA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII

5.1 Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii kuitembelea rasmi Taasisi hii ili kuifahamu na kuona huduma zinazotolewa na Taasisi.

5.2 Kamati ya Huduma za Jamii kupitia Mikataba iliyopendekezwa na ikiona Mikataba hiyo inafaa basi Kamati isaidie kuishawishi/kuishinikiza Wizara ya Afya kutoa ushirikiano na kuridhia Mikataba iliyoainishwa hapo juu.

5.3 Baada ya kuridhia Mikataba hiyo hapo juu Wizara/Serikali ilete wagonjwa kutibiwa kwenye Taasisi ya THI kwa vile Taasisi itakuwa na uwezo mkubwa wa kimataifa. Tatizo la kudai kuwa Taasisi haina Wataalam na vifaa litakuwa limekwisha.

5.4 Kushawishi na kusaidia Taasisi zingine za Serikali kuingia ubia na THI. THI iko tayari kushirikiana na kuingia ubia na Taasisi za Serikali kama Hospitali ya Taifa Muhimbili, Shirika la Hifadhi za Jamii (NSSF), n.k.

5.5 Ikiwezekana majengo haya ya NSSF ipewe Taasisi ya Moyo Tanzania kwani lengo kwa wote ni kuwahudumia wananchi na kulijenga taifa letu. Taasisi iko tayari kutoa huduma kwa wagonjwa kwa gharama ya kufidia gharama za pango. Hii ikiwa na maana kuwa baadhi ya fedha itakayolipwa na Serikali kwa ajili ya wagonjwa itakwenda moja kwa moja kwenye Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF).

Ni matumaini yangu kuwa Taarifa hii fupi itasaidia kutoa hali halisi na mwanga kuhusu maendeleo ya Taasisi yetu ya Tiba ya Magonjwa ya Moyo ya Tanzania (THI).

Natanguliza shukrani zangu za dhati kwa ushirikiano wenu.

MUNGU IBARIKI THI! MUNGU IBARIKI TANZANIA!

Wako katika Ujenzi wa Taifa,

Dr. Ferdinand B. Masau
MWANZILISHI NA MKUU WA TAASISI, THI
4 Julai, 2008